DIGNITY

Uzima

Toleo la 19
hello@dignityonline.org.uk
+447340 573 937

Kujenga Sawasawa

Matayo 7 inaeleza historia ya watu wawili waliojenga nyumba zao. Mmoja alijenga juu ya mwamba, na mwingine juu ya mchanga. Dhoruba kubwa ikapiga nyumba zao. Upepo na mvua zikapiga ukuta. Ile iliyojengwa juu ya mchanga ikaanguka. Ile iliyojengwa juu ya mwamba ikabaki imara.

Kuweka msingi imara ni jambo la muhimu sana. Ni vitu vya mwanzo tunaweka chini wakati tunajenga nyumba. Inagua kwa ujumla nguvu ya nyumba.

Yesu alisema watu wanaofanyia kazi mafundisho yake wanafananishwa na mtu aliyejenga nyumba yake juu ya mwamba. Mwamba ni imara na wanaweza 'kujenga' juu yake kwenye maisha yao yote – maana inawapa msingi uliyo imara. Wakati 'mafuriko' yanapokuja, mambo magumu na changamoto ya maisha, wataweza kusimama imara ndani ya Yesu bila kupoteza matumaini. Yesu pia aliwaonya wale watu wasiofanyia kazi mafundisho yake wanafananishwa na mtu aliyejenga nyumba yake juu ya mchanga. 'Mafuriko' yalipokuja, hawakuwa na msingi imara wa kusimama juu yake na hii ikawafanya kuwa thaifu na kuadhirika.

Hivyo pia, kama Kikundi cha Uzima tunahitaji msingi imara. Tunapaswa pia kujenga kwa hekima, huku tukitazama Biblia itusaidie. Hoja zingine za Maisha zitavumbua msingi uliyo imara na kujenga matofali aliyotoa Yesu kwenye Kikundi cha Uzima. Hii itatusaidia sisi kujua namna, pamoja na Mungu, tunaweza kuwafikia wengine na kuleta tofauti kwa jumuia inayotuzunguka.

Msingi wetu uliyo imara uko ndani ya MUNGU akifanya kazi pamoja nasi, ndani na kupitia watu wake. Kwenye kitabu cha Isaya 61:3-4 Mungu anawaita watu aliyowaokoa 'mwaloni (miti mikubwa) ya haki'. Anasema kuwa nao watajenga mahali pa kale palipoharibiwa watapainua mahali palipokuwa ukiwa zamani watatengeneza miji iliyoharibiwa. Hii inatuonyesha sisi kuwa Mungu amechagua kufanya kazi ndani na kupitia watu wake.

Pamoja na hizi mahali, tunaweza kujenga nguzo za pembe nne kushikilia paa: kufanya kazi pamoja, kutumia vifaa sahihi, kufanya kazi sehemu sahihi na kuamini msaada sahihi.

Paa la nyumba yetu huwakilisha maisha ya baadaye. Kwa sasa, tuseme tu kwa wepesi kuwa Mungu na watu wake hufanya kazi kutangaza ujumbe na uwepo wa Mungu, na kuleta upendo wa Mungu na kuwajali watu.

Tutaendelea kugundua kila moja ya mawazo haya zaidi kwenye hoja zinazokuja za Maisha.


Zingatia:

Pamoja na marafiki:

- Angalia majengo yanayokuzunguka kwenye kijiji chako. Unaweza kuweka alama ya msingi kwenye moja wapo? Unagundua nini?
- Zungumza kuhusu wakati mtu alipojenga nyumba. Jadilini kwa nini msingi ni kitu cha muhimu na kile wanachofanya.
- Tazama ndani ya Biblia kwa vifungu inayohusu misingi. (Unaweza kutazama Matayo 7:24-29, Isaya 28:16 au 1 Wakorinthio 3:10-17.

Omba:

1) Yesu atakusaidia kuweka maneno yake kwenye matendo na kukupa misingi iliyo imara.
2) Watu wa Mungu watafanya kazi pamoja na 'kujenga vizuri'



Edward* aliamka usiku mmoja kusikia mvua kubwa na upepo ukipiga paa na kuta zake. Akashangaa, aliona kuta zilikuwa zikiinama ndani na kupasuka. Edward aliiamsha familia yake na wakakimbia nje ya nyumba kabla ya nyumba kuanguka. Siku iliyofuata Edward aligundua tatizo. Misingi ilikuwa imewekwa kwa nyumba, lakini kuta hazikuwa juu ya misingi, zilikuwa juu ya mchanga. Mchanga uliloana wakati wa dhoruba na haukuweza kubeba uzito wa kuta, kwa hivyo zilianguka.

- Edward,* Zambia

Labda unauliza:

Je, Mungu kweli anafanya kazi na watu?

Katika Biblia tunaona hadithi nyingi za Mungu akifanya kazi na watu wanaohisi kwamba hawana uwezo wa kutosha, nguvu za kutosha, au akili za kutosha. Soma hadithi zao ili utiwe moyo!

Kwa rasilimali zaidi za Dignity tembelea:
www.dignityonline.org.uk/library

*Jina limebadilishwa kulinda siri za mtu

Dignity ni Shirika la ufadhili la kibinafsi lililosajiliwa Nambari. 1122656. Dignity. (Ulimwenguni) ni Kampuni inadhibitiwa kwa Uhakiki, imesajiliwa Uingereza, Nambari. 6394480 Dignity Zambia. Kampuni ya Faida kwa Umma katika Jamhuri ya Zambia Nambari. 117117. Maandiko Matakatifu ya Mungu Yaitwayo Biblia. Published jointly by The Bible Society of Tanzania and The Bible Society of Kenya. Imetumika kwa idhini. Haki zote zimehifadhiwa ulimwenguni kote.

Swahili